**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT.PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA KONGAMANO LA VIONGOZI WA DINI WA KAMATI ZA AMANI NA JUMUIYA YA MARIDHIANO TANZANIA KUHUSU MAADILI NA AMANI

**DAR ES SALAAM**

**TAREHE 28 NOVEMBA, 2022**

***Sheikh Dkt. Alhad Mussa Salum, Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Kamati za Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania;***

***Mhe. Hamad Y. Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi;***

***Mheshimiwa Ludigija - DC Ilala kny ya Mkuu wa Mkoa wa DSM;***

***Mwakilishi wa Mufti wa Tanzania;***

***Mchungaji George Fupe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati za Amani Tanzania;***

***Mchungaji Dkt. Eliyas Silayo, Makamu Mwenyekiti Jumuiya ya Maridhiano Tanzania;***

***Mzee Azim Dewji, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Jumuiya ya Maridhiano Tanzania;***

***Mchungaji Dkt. Israel Maasa, Katibu Mkuu, Jumuiya ya Maridhiano Tanzania;***

***Mufti wa Jamhuri ya Kenya;***

***Wajumbe wa Bodi ya wadhamini, Jumuiya ya Maridhiano Tanzania;***

***Wajumbe wa Kamati Kuu Jumuiya ya Maridhiano Tanzania;***

***Wajumbe wa Kamati za Maadili na Jumuiya ya Maridhiano kutoka mikoa yote nchini Tanzania;***

***Chief wa Wamasai;***

***Washauri wa Kamati za Amani Tanzania; Makundi yote yaliyowakilishwa hapa;***

***Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wakiongozwa na Mnadhimu Mkuu wa JWT - Lt. Gen Salum Haji Othman;***

***Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

***Akina Mama wote - walezi wakuu wa maadili;***

***Asalam Aleykum…***

***Bwana Yesu Asifiwe…***

***Tumsifu Yesu Kristu…***

***Mwanakondoo ameshinda…***

Tanzania Yetu! Amani kwanza

Napenda kuanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai na kibali cha kukutana hapa siku hii. Napenda kuzishukuru Kamati za Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania kwa kukubali mimi nije kushiriki Kongamano hili kwa niaba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye hakuweza kujumuika nanyi katika tukio hili muhimu kwa Taifa kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa aliyonayo. Mheshimiwa Rais alifurahi sana kusikia mmeandaa Kongamano hili na naomba mpokee shukrani zake za dhati kwa kuendelea kuliombea Taifa letu amani, umoja, utulivu na maendeleo.

Aidha, nami kwa niaba ya Serikali napenda kuzipongeza Kamati za Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania kwa kazi nzuri mnayoifanya ambayo imesaidia kujenga maelewano baina ya viongozi na waumini wa dini mbalimbali na kuhimiza amani miongoni mwa watanzania. Serikali inathamini sana mchango wenu huo ambao umeendelea kuifanya nchi yetu kuwa mfano wa kuigwa ndani na nje ya Bara la Afrika kama Taifa la Amani, umoja, utulivu na kimbilio la walio wengi. Naomba kukiri kuwa Mheshimiwa Rais aliponipa jukumu hili nilipata kigugumizi! Nilijiuliza nitasema nini na Viongozi ambao ndio walimu wetu na walezi wa maadili katika jamii.

***Ndugu Viongozi,***

Viongozi wa dini mnayo nafasi ya kipekee na mchango mkubwa katika kufundisha na kulinda maadili mema na kukemea mwenendo mbaya katika jamii yetu. Naamini mmechagua kujadili suala la maadili kwa kuwa ni dhahiri, hivi sasa Taifa letu na dunia kwa ujumla inapitia katika changamoto nyingi za mmomonyoko mkubwa wa maadili kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo malezi dhaifu na utandawazi holela. Hivyo, sisi kwa upande wa Serikali tungependa viongozi wa dini mwendelee kutusaidia kupaza sauti kukabiliana na mmomonyoko wa maadili. Naomba niseme baadhi ya matukio na mienendo isiyofaa kama ifuatavyo: Naomba sana radhi pale nitakapotumia lugha au maneno ambayo hayapendezi masikioni penu!

**Kwanza, ni Ukatili wa Kijinsia:** katika Taifa letu, tumeendelea kushuhudia matukio ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto yakiripotiwa mara kwa mara sehemu mbalimbali za nchi yetu. Takwimu kutoka Jeshi la Polisi kwa mwaka 2021 zinaonesha kuwa makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114). Najiuliza hofu ya Mungu

imepotelea wapi? Kwa maoni yangu haya yote yanatokana na mmomonyoko wa maadili katika familia na jamii yetu kwa ujumla. Ni lazima kama jamii tutambue haki za msingi za mtoto ikiwepo haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa na haki ya kutobaguliwa. Watoto ni hazina muhimu kwa Taifa na miongoni mwao ndipo tunatarajia kupata viongozi wa Taifa letu, Viongozi wa dini na wataalam katika katika fani mbalimbali. Hatuna budi kuwa na mifumo imara ya ulinzi kwa watoto wetu katika ngazi ya familia, mtaa, mashuleni, madrasa, vyuoni na sehemu nyingine ili kulinda haki na ustawi wa watoto wetu. Kila mmoja ana jukumu la kuhakikisha watoto wanakua katika mazingira salama na katika maadili mema. Imefika wakati sasa tukemee vitendo hivi bila woga wala aibu na kuchukua hatua na katika jambo hili tusilindane! Tuwafichue wahusika. Napenda nitumie fursa hii kukemea vikali ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto wa kike na kiume kote nchini. Nawahakikishia kuwa, Serikali itaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wale wote wanaojihusisha na vitendo hivi. Navitaka vyombo vyote vya dola kuongeza nguvu kupambana na ukatili wa watoto.

Kadhalika, ukatili dhidi ya wanawake nao umekithiri na wote tunafahamu ni kinyume na maagizo ya Mwenyezi Mungu katika dini zote, na ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo jumuishi na endelevu. Ukatili kwa mama zetu katika nchi yetu unachukua sura ya vipigo, usafirishaji haramu wa binadamu, ukatili wa kingono, ndoa za utotoni, ukeketaji na mauaji. Sote hapa tunasikia au kusoma juu ya ukatili uliopitiliza kwa wanawake kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii jinsi wanawake wanavyonyanyaswa, kudharauliwa, kupigwa na hata kuuawa kinyama. Kwa mfano, matukio ya unyanyasaji dhidi ya wanawake kwa mwaka 2021 yalikuwa ni 20,897 na mwaka 2020 yalikuwa 28,126 na ninaamini zipo kesi zaidi ambazo hazikufika kwenye vyombo vya dola. Mkiwa kama viongozi wa dini, naamini ninyi ni mashahidi wazuri kwa yanayotokea katika jamii yetu. Hivyo, ninawasihi muendelee kushirikiana na Serikali kupaza sauti zenu zinazoheshimika kukemea vitendo hivi viovu na pia kukataza mila na desturi zote katili, zinazodhalilisha au kumnyima mwanamke haki zake za msingi. Si hivyo tu, hivi karibuni tumeanza kusikia baadhi ya wanaume kunyanyaswa na wake zao hadi wameanzisha chama cha kuwaunganisha kupinga ukatili na dhuluma wanazofanyiwa. Hili nalo halipaswi kufumbiwa macho.

**Pili, Mimba za Utotoni na ongezeko la Watoto wa Mitaani:** tatizo la mimba za utotoni na Watoto wa mitaani bado lipo nchini na sababu kubwa zinazotajwa kusababisha ni malezi, utandawazi na hali ya umaskini katika kaya. Baadhi ya wazazi wameacha kutimiza jukumu lao muhimu la malezi kwa watoto

na vijana kwa visingizio mbalimbali ikiwemo kuvurugika kwa ndoa ambapo watoto na vijana wetu hulazimika kulelewa katika mazingira yasiyoridhisha. Utandawazi na hali ya umaskini katika kaya nazo zinatajwa kuchangia baadhi ya Watoto kuingia katika matendo maovu na makundi hatarishi ambapo matokeo yake ni pamoja na kuacha shule na kuwa Watoto wa mitaani, kufanya mambo yasifaa katika jamii na yasiyompendeza Mwenyezi Mungu, kama kutumia madawa ya kulevya, vitendo vya wizi, ujambazi, kukosa heshima, ulevi, kufanya vitendo vya ngono hata juu ya makaburi! ni mambo ya kutisha. Ni laana. Mimi naamini kwa dhati kuwa vijana wetu wakifundishwa mila na desturi sahihi na kushika mafundisho ya dini, na wakawa na hofu ya Mwenyezi Mungu, maovu mengi yatapungua. Hivyo niwasihi ninyi Viongozi wetu wa dini zote, Viongozi wa Kimila na Wazee tusaidiane kulea watoto na vijana wetu kimaadili kwani wao ndio warithi wa Taifa letu. Tukiwaandaa vyema, mustakabali wa nchi yetu na watu wake utakuwa kwenye mikono salama.

**Tatu, ni Ukahaba:** jambo hili limezidi kuenea, lakini tabia hii haikubaliki katika mila na desturi za kiafrika na katika dini zote. Wazazi kutowajibika ipasavyo katika malezi ya Watoto wao ni moja ya sababu zinazotajwa kuwa chanzo cha tatizo hili. Wengi wa  hukiri kuwa jambo hilo walifundishwa na ndugu, jamaa, marafiki, wafanyakazi wa majumbani au wageni waliokuwa wakifika katika familia husika. Tunawaomba vingozi wetu wa dini zetu zote mtumie majukwaa yenu kutusaidia kupaza sauti kufundisha waumini wenu na kukemea vikali jambo hili kwani ni kinyume kabisa na utamaduni wetu na madhara yake kiuchumi na kijamii ni makubwa mno.

**Nne, Biashara ya Dawa za Kulevya.** Janga hili bado lipo nchini na linaathiri sana afya na ustawi wa watu wetu, hasa vijana ambao ndio nguvu kazi muhimu ya Taifa.  Wengi wetu tumeshuhudia jinsi vijana wengi walivyopoteza kabisa mwelekeo wa maisha na hata wengine wamekufa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, tatizo hili kwa kiasi kikubwa linaathiri afya za vijana wetu, jamii, uchumi na kuhatarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Baadhi ya vijana wetu wamekuwa zezeta na wengine kujihusisha na makundi ya kihalifu. Hivyo, kupitia Kongamano hili, napenda nitoe wito kwenu na Watanzania wote kwa pamoja kushiriki katika mapambano haya kwa kutoa elimu kwa jamii kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya, na pia kutoa taarifa na kuwafichua wote mnaowafahamu au kusikia tetesi kuwa wanajishughulisha na biashara hii haramu.

**Tano, Mmomonyoko wa Maadili sehemu za Kazi hususan Rushwa na Ufisadi.** Vitendo vya rushwa na ufisadi wa mali ya Umma ni miongoni mwa mambo yanayohatarisha na kutishia uhai, ustawi, tunu, uchumi na msingi wa maendeleo ya nchi. Inasikitisha kuona taasisi zinazoongoza kwa shutuma za rushwa ni taasisi ambazo zinategemewa na wananchi kuwa mstari wa mbele kutoa na kutetea haki. Halikadhalika, wanaojihusisha na ufisadi ni viongozi na watumishi wa umma ambao ni waumini wa dini mnazoziongoza na hivyo walitarajiwa kuwa waadilifu na mfano wa kuigwa katika jamii. Viongozi wa dini tusaidieni huko makanisani na misikitini kukemea rushwa, wizi na tamaa ya kujilimbikizia mali haraka haraka kwa njia zisizo halali kwani naamini Mungu hapendezwi na sadaka inayotokana na rushwa, ufisadi au ujambazi. Ni vyema tujikumbushe kuwa, jukumu la kupambana na rushwa pamoja na ufisadi si la Serikali peke yake, bali ni letu sote. Wakati Serikali ikijitahidi kuimarisha mifumo ya utoaji huduma ili kudhibiti vitendo vya rushwa na ufisadi, nawasihi sana viongozi wetu wa dini kukemea vitendo vya aina hiyo na kuendelea kuwaelimisha wananchi madhara ya kutoa na kupokea rushwa pamoja na kushiriki kuhujumu mali za umma. Serikali itaendelea kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayejihusisha na vitendo hivi bila kujali cheo au nafasi yake katika jamii.

***Sita, Uharibifu wa Mazingira na Utupaji Taka Ovyo***

Napenda nitumie fursa hii kuwasihi kupitia majukwaa yenu muendelee kuisaidia Serikali katika kuwaelimisha waumini kuhusu usafi na uhifadhi wa mazingira. Hivi karibuni nchi yetu ilikumbwa na uhaba mkubwa wa maji katika maeneo mengi ambao kwa kiasi kikubwa ulitokana na ukame uliopelekea kukauka kwa vyanzo vya maji hali iliyochangiwa zaidi na tabiawatu kupitia shughuli mbalimbali ambazo zina athari kwa mazingira kama uchomaji moto hovyo, ukataji miti kwa ajili ya mbao na mkaa, shughuli za kilimo pamoja na utupaji wa taka hovyo katika vyanzo vya maji na taratibu nyingine zisizofaa kama kutapisha vyoo wakati mvua zinaponyesha mijini. Nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wa dini mtusaidie kuongeza msisitizo kwa waumini wetu kuhusu kudumisha usafi na uhifadhi wa mazingira na kuhakikisha kwamba vijana wetu wanakua katika maadili mema ya kupenda kutunza mazingira kwa faida ya sasa na kizazi kijacho.

***Ndugu Viongozi***

Serikali inatambua na kuthamini sana mchango wa Dini zote katika kujenga maadili mema ndani ya jamii zetu. Serikali ina matarajio makubwa sana na

Viongozi wa Dini zote nchini katika kukuza maadili mema kuwa role models/mfano wa kuigwa na kukemea yale yasiyo mema hususan kwa:

(i) kufundisha watoto, vijana na familia maadili mema kwa kupitia mawaidha/mahubiri kwa maneno au vitendo na kukemea yale yasiyo mema pale yanapotokea;
  - nguo zisizositiri mwili na staha (mgongo wazi, fupi, mtepesho)
  - Lugha za matusi/kihuni
  - Mila potofu

(ii) kusaidia waathirika wa ukosefu wa maadili kwa hali na mali na kutoa ushauri nasaha ili kuwawezesha warejee kwenye mwenendo ulio mwema katika jamii;

(iii) Kuvisaidia na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kulinda na kusimamia maadili katika Taifa letu; na

(iv) Kuiombea nchi yetu Amani & ustawi wa Watanzania.

***Ndugu Viongozi***

Ninapata kigugumizi kidogo kusema nanyi Viongozi wangu wa dini kuhusu wajibu wenu, maana kumwambia mkubwa wako madhaifu yake si jambo rahisi. Natangulia kuomba radhi kama nitawakwaza kwa hili! Viongozi wa dini ni kioo cha jamii hususan katika suala la maadili. Kulingana na mafundisho ya dini zetu, viongozi wa dini ni wawakilishi wa Mwenyezi Mungu hapa duniani. Ninyi ndio mnaotufundisha na kutuelekeza kwa Mungu kulingana na mafundisho ya vitabu vitakatifu na matendo yenu pia. Kwa ajili hiyo, jamii inawatarajia kuwa mtakuwa kielelezo cha maadili mema na mfano wa kuigwa. Hii ndiyo sababu inapotokea kiongozi wa dini amekosea au kuenenda kinyume na maadili, jamii inapata shida sana kumuelewa. Hivyo ninyi kama Viongozi wa dini ni muhimu kujiepusha na migogoro ndani ya Taasisi zenu. Sisi viongozi wa Serikali tunasikitika kupokea taarifa za migogoro inayotokea ndani ya taasisi za dini. Baadhi yenu mmekuwa mkikimbilia Serikalini na Mahakamani kushitakiana kwa migogoro ambayo mngeweza kuzungumza na kuitatua wenyewe. Kiini cha migogoro hii ukiangalia kwa karibu ni uchu wa madaraka, ubinafsi, uchu wa fedha, matumizi mabaya ya mali za taasisi za dini na ukiukwaji wa katiba za taasisi zenu za dini. Kwakweli jambo hii linaleta taswira mbaya kwenu viongozi wa dini na taasisi mnazoziongoza. Jamii inashindwa kuwaelewa kwani kama viongozi wetu mnadhamana ya kutulea kimaadili na kutuonesha njia iliyo sahihi. Napenda kwa unyenyekevu kabisa nitumie fursa hii kuwasihi sana viongozi wangu wa dini zote kuepuka migogoro, lakini pindi inapotokea basi tuhakikishe tunaisuluhisha mapema kwa kuzingatia sheria, miongozo na taratibu zinazokubalika. Ninaamini

ninyi mkizingatia maadili mema itakuwa rahisi kwenu kufundisha, kukaripia na kuionya jamii bila kunyooshewa vidole. Serikali kwa upande wake itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi na madhehebu yote ya dini nchini.

***Ndugu Viongozi,***

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, ni vema nisemee kidogo baadhi ya changamoto mlizozieleza. Kuhusu hili la baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutotoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati za Amani na Jumuiya za Maridhiano Tanzania, napenda nichukue fursa hii kuwakumbusha tena Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote kuhakikisha wanatoa ushirikiano wa kutosha kwa kamati hii. Waheshimiwa Viongozi wangu wa dini pale mtakapokuwa hampewi ushirikiano bila maelekezo yaliyonyooka, basi milango iko wazi tujulisheni ili tukwamue. Aidha, kuhusu suala la kupatiwa Ofisi na vitendea kazi naomba niseme tu kwamba Serikali itashauriana na Wadau mbalimbali kuona namna bora ya kutatua changamoto hiyo. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ulifanyie kazi.

Mwisho kabisa napenda kuwasihi viongozi wetu wa dini kuendelea kuliombea Taifa na sisi viongozi na watumishi wa Serikali tunaohudumu hivi sasa na mfanye hivyo bila kuchoka ili tuweze kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi na watu wake tuliyojiwekea. Niwaombe muendelee kutumia nafasi zenu kufundisha, kuonya na kushauri pale inapobidi kwa maslahi ya kustawisha Taifa letu. Asanteni sana kwa fursa hii nzuri (ukiondoa mwaliko wa Sheikh Alhad kuongeza mwanachama wa wake wenza)!! Asanteni kwa kumtia moyo Rais na kumwombea

Baada ya kusema haya, kwa niaba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nawatakia Kongamano lenye mafanikio na tunaomba mtupatie mapendekezo yatakayo tokana na majadiliano yetu na sasa nafurahi kutamka kuwa **Kongamano la Viongozi wa Dini wa Kamati za Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania kuhusu Maadili limefunguliwa rasmi.**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza!!**